| جمهورية مصر العربية<br>وزارة الأوقاف | ٢٩ شعبان ١٤٤٣ هـ<br>١ أبريل ٢٠٢٢م |
|---|---|

(١)

Je, Tunaupokeaje Mwezi Mtukufu wa Ramadhani?

Prof.Ayman Alasar

Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mola wa viumbe vyote, anayesema katika Kitabu chake Kitakatifu:

{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِنْ قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ}

{Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama walivyoandikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kumcha Mwenyezi Mungu}.

Na ninashuhudia kuwa hakuna Mungu mwingine aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, peke yake hana mshirika wake. Na ninashuhudia kuwa Bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni Mja na Mjumbe wake. Anasema S.A.W: Mtu yoyote atakayeufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa Imani na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, basi atasamehewa madhambi yake aliyoyafanya.

Ewe Mola wetu msalie na umbariki yeye na Jamaa zake na Maswahaba wake wote. Na mwenye kuwafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.

Na baada ya utangulizi huu

Katika fadhila za Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa waja wake, ni kuwajaalia msimu wa misimu ya Kheri nyingi, ndani yake tunu zake zinafululiza kutolewa, na rehma nyingi huteremka, na malipo huwa makubwa. Anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika Mola wenu ana katika masiku ya nyakati zenu kutoa tunu zake, basi jihusisheni na masiku hayo, kwani huwenda mmoja wenu akazipata tunu za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kumfanya asiwe mwovu tena milele. Na hakika miongoni mwa misimu hiyo iliyo bora kabisa kwa kuwapambazukia waumini, na yenye baraka na fadhila nyingi, ni mwezi mtukufu wa Ramadhani, uliobarikiwa; Mwezi unaozingatiwa kuwa ni Bwana wa Miezi mitukufu na siku zake ni siku Bora na zenye heri zaidi, na nyusiku zake ni katika nyusiku zilizo safi na zenye kutwaharika. Na Mtume S.A.W alikuwa akitoa habari njema kwa kuingia Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na alikuwa akiwabashiria Maswahaba wake R.A, kuhusu upaji huu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu. Kutoka kwa Abu Huraira, R.A, amesema: Mtume S.AmW anasema: Umekujieni Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Mwezi wa, Mwezi uliobarikiwa, Mwenyezi Mungu Mtukufu amekufaradhishieni funga yake, ndani ya Mwezi huu, Milango ya Mbinguni hufunguliwa, na hufungwa Milango ya Jahannamu, na Mashetani waovu hufungwa, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuna kuna Usiku ulio Bora kuliko Miezi elfu moja, na yoyote atakayenyimwa Kheri zake atakuwa amenyimwa.
Na Maswahaba wake Mtume S.A.W, walikuwa wanamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu awafikishe katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na awasaidie katika kufanya kazi njema ndani yake. Anasema Bin Rajab Mola amrehemu: Wengi miongoni mwa wema walikuwa wanamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu miezi sita, awafikishe Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kisha wanamwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa miezi mingine sita awakubalie waliyoyafanya ndani ya mwezi huo mtukufu wa Ramadhani. Na anasema Yahya bin Abu Kathiir: Miongoni mwa Dua zao, ilikuwa: "Ewe Mola wangu nifikishe salama katika Mwezi Mtukufu wa

Ramadhani na uupokee Mwezi huo kutoka kwangu kwa kuukubali. Na kutoka kwa Jabir bin Abdillah R.A, Anasema: Kwamba Mtume S.A.W, alikuwa akipanda katika Membari ya Msikiti, na alipopanda ngazi ya Kwanza akasema: Amin. Kisha akapanda ngazi ya pili na akasema tena: Amin: Kisha akapanda ngazi ya tatu na akasema tena Amin. Na Maswahaba R.A, wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu, tumekusikia ukisema: Amin mara tatu? Mtume S.A.W akasema: Nilipopanda ngazi ya Kwanza alinijia Jiburilu na akaniambia: "Mja yoyote atakuwa amefanya kosa kubwa sana iwapo ataudiriki Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kisha akaumaliza, akiwa hajasamehewa madhambi yake. Mimi nikasema Amin..." Wakati sisi tunajiandaa kumpokea Mgeni huyu adhimu - baada ya siku chache - tunapwaswa kumfuata Mtume S.A.W, na Maswahaba wake watukufu, na kuwaiga wao katika Ibada zao na matendo yao ndani ya Mwezi huu wa ramadhani, uliobarikiwa. Muislamu anapaswa kuleta nia na kuifanya upya, kwani kwa nia hiyo, Waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu wanatofautiana mbele ya Mola wao Mtukufu, kwani hiyo Nia ndio siri ya kukubaliwa matendo yao. Anasema Mtume wetu S.A.W: Hakika ya Matendo ni kutokana na Nia zake, na Hakika ya kila Mja ana kile alichokinuia, na yule ambaye kuhama awake kulikuwa ni kwa ajili ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake, basi kuhamaka kwake ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake, na yule ambaye kuhama kwake kulikuwa ni kwa ajili ya kuipata Dunia, au kumpata Mwanamke wa kumuoa, basi kuhama kwake ni kwa ajilivalichokinuia kukihamia. Na kutoka kwa Abu Huraira R.A, amesema: Mtume S.A.W anasema: Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Kila kazi ya mwanadamu ni yake isipokuwa Swaumu ni yangu na mimi ndiye mwenye kuilipa. Na Swaumu ni Kinga, na inapokuwa siku ya mmoja wenu amefungua, basi asimwingilie mke Wake, na wala asipige makelele hovyo, na iwapo Mtu yoyote atamtukana au kutaka kugombana nae na aseme: Hakika mimi ni mja niliefunga. Na ninaapa kwa yule ambaye Nafsi ya Muhammad iko mikononi mwake, hakika harufu ya mdomo wa Mtu

aliyefunga ni bora mbele ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuliko harufu ya Miski.

Vile vile inampasa Mwislamu katika Mwezi Mtukufu wa ramadhani aongeze kila aina ya utiifu na matendo mema, na kufuata yale aliyoyausia Mtume S.A.W na alikuwa akiyafanya, kama vile kuharakisha kufuturu, na kuchelewesha ulaji wa daku. Ambapo anasema Mtume wetu S.A.W: Umma wangu utaendelea kuwa katika heri iwapo utaendelea kuharakisha kufuturu na kuchelewesha kula Daku.
Na anasema Mtume S.A.W: Kuleni Daku kwani Hakika katika kula Daku kuna baraka. Vile vile ni lazima kujiepusha na Ubadhirifu katika vyakula na vinywaji.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

{وَكُلُوا وَاشْرَبُوا وَلا تُسْرِفُوا إِنَّهُ لا يُحِبُّ الْمُسْرِفِينَ}
{...na kuleni, na kunyweni na wala msifanye ubadhirifu. Kwa hakika Yeye hapendi wanao fanya israfu}.

Na anasema Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: Mwanadamu hajawahi kulijaza tumbo lake chakula isipokuwa Shari, mwanadamu hutosheka na uchache wa chakula kinachomwezesha kuishi; na kama awezi kukwepa kula: Basi theluthi moja iwe ya chakula chake, na theluthi moja ya kunywa, na theluthi moja ni ya kupumulia kwake. Uzuri ulioje kwa matajiri kuhisi mahitaji ya mafukara ndani ya Mwezi huu Mtukufu wa ramadhani, kwani Mwezi Mtukufu wa ramadhani ni Mwezi wa utoaji, upaji na ukarimu, Mwezi ambao maana halisi ya huruma, upole ulaini wa moyo hujengeka ndani yake kwa ajili ya Mayatima, Wajane, Mafukara na Masikini, kwa njia zote za kuleana na ikawa hiyo ni sababu ya kuingiza furaha na tabasamu

kwao kwa kufuata njia ya Mtume S.A.W katika hali zake zote, na hasa katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kutoka kwa Bin Abas R.A, amesema: Mtume S.A.W alikuwa Mbora wa Watoaji, na ubora wake wa kutoa ulikuwa ukionekana ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, anapokutana na Jiburilu, na alikuwa anakutana naye kila siku usiku katika nyusiku za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na anafundisha Qurani. Mtume S.A.W alikuwa Mwingi wa kutoa kuliko upepo wa kimbunga. Na hili halimaanishi utoaji wa mali tu, bali Maana yake ni pana zaidi kuliko hivyo na inakusanya Wema, Kuunganisha undugu, Kuhurumia na Kuwapenda watu, na kuzichunga haki zao na Wajibu wa kila mtu. Kama ambavyo Mwislamu anatakiwa kuzidisha Ibada kama vile Kusoma Qurani kwa wingi, na kuzizingatia maana za aya za Quran, na kuswali swala ya Usiku ambapo anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakaye swali Tarawehe ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa Imani na Kumtegemea mwenyezi Mungu Mtukufu, basi atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia. Na anasema Mtume S.A.W: Mtu yoyote atakaye swali Tarawehe ndani ya Usiku wa Cheo, kwa Imani na kwa kumtegemea Mwenyezi Mungu Mtukufu, atasamehewa madhambi yake yote yaliyotangulia. Na kutoka kwa Bi Aisha R.A, kwamba Mtume S.A. siku moja usiku alitoka na akaswali Msikitini, na Maswahaba wakaswali naye swala yake hiyo na kisha wakaizungumzia, na watu wakakusanyika kwa wingi na wakaswali naye, na walipoamka wakazungumza, na watu wa  Msikiti huo wakajaa usiku wa tatu, Mtume S.A.W, akatoka na wao wakaiswali Swala yake, na ulipowadia usiku wa nne Msikiti ukajaa watu wake mpaka Mtume S.A.W akatoka kwa ajili ya kwenda kuswali swala ya alfajiri, na baada ya kumaliza kuiswali Swala yake, watu walimwendea, akatoa Shahada ya kumalizia Swala kisha akasema: Ama Baad. Hakika mambo yalivyo, hali yenu haikufichika kwangu, lakini mimi nilichelea msije mkafaradhishiwa na kisha mkashindwa kuiswali Swala hiyo. Kisha Bwana wetu Umar R.A akaona wakati wa Ukhalifa wake, awakusanye Waislamu waswalishwe na Mtu mmoja. Na kutoka kwa Abdul

Rahmani bin Abdul Kaariu, kwamba yeye amesema: Nilitoka pamoja na Umar bin Khatwab R.A, usiku wa Ramadhani tukaelekea Msikitini, na tukawakuta watu wametawanyika na kugawanyika na kila mmoja anaswali peke yake, na mwingine anaswali huku watu kadha wakimfuata, Bwana wetu Umar akasema: Mimi ninapendekeza kama ningewakusanya watu hawa kwa Msomaji mmoja ingekuwa bora zaidi, kisha akakusudia hivyo na akawakusanya kwa Msomaji mmoja ambaye ni Bwana wetu Ubayyah bin Kaabi R.A, kutokana na Shime yake ya kuendeleza Ibada hii ya Swala ya Tarawehe na Umoja wa Waislamu.

Swaumu ya kweli ni ile ya kujizuia na aina zote za maaswi na madhambi, ni wangapi wafungao hawana isipokuwa funga na Njaa na Kiu! Anasema Mtume S.A.W: Huwenda ikawa kwa Mfungaji anachokipata kutokana na swaumu yake ni Njaa na Kiu tu, huwenda anayeswali Tarawehe anachokipata ni kuswali kwake usiku.
Na anasema Mtume S.A.W: Mtuasiyeacha uzushi wa maneno na kuufanyia kazi, basi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hana haja yoyote ya kuacha kula na kunywa kwake. Naye Jabir bin Abdillah R A, amesema: Utakapofunga basi Masikio yako yafunge, Macho yako yafunge, na Ulimi wako ufunge na kujiepusha na Uongo na ysliyokatazwa na kuharamishwa, na ahca kumfanyia maudhi mtumishi wako, na uwe na Unyenyekevu, na Utulivu katika siku yako ya swaumu yako, na wala usiifanye siku yako ya kula na siku yako ya kufunga kuwa sawa sawa, na apupie Mwislamu mpaka siku yake ya swaumu iwe funga ya kweli na mpaka matunda yake yanayotarajiwa yapatikane kutokana na swaumu yake hiyo, na Matunda hayo ni kumcha Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Na ni juu yetu kutambua kuwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani uliobarikiwa ni Mwezi wa bidii na jitihada pamoja na kuchapa Kazi, kwa hiyo jitihada zetu na Kazi zetu zisipungue katika Mwezi Mtukufu

wa Ramadhani kwa kulinganisha na Miezi mingine, kwa Madai ya uchovu na Tabu. Kwani watu wengi huelekea katika ulegevu na uvivu, na hulala mchana wa Ramadhani kwa wingi, jambo ambalo husababisha kuzorotesha kwa masilahi ya watu ndani ya Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani. Na yote haya ni kinyume kabisa na lengo kuu la Funga ambalo Mwenyezi Mungu Mtukufu ameifaradhisha Ramadhani kwa ajili yake, ambalo ni Uchamungu.
Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**{يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الصِّيَامُ كَمَا كُتِبَ عَلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ}**

{Enyi mlio amini! Mmeandikiwa Saumu, kama waliyo andikiwa walio kuwa kabla yenu ili mpate kuchamngu}.

Kwa hiyo, Uchamungu hauji kwa Uvivu na Ulegevu; bali huja kwa Ibada nyingi na Kazi, Usafi wa Nia na kujichunga kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu.
Na ikiwa moja kati ya sifa maalumu za mwenye swaumu ni kujichunga kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, hakika Sifa hii inapelekea Mwenyezi Mungu Mtukufu kufuatilia na kuchunga utekelezaji wa haki ya kazi, kwani yule ambaye anazichunga swala zako na funga zako na kujizua kwako na kula na kunywa, ndiye huyo huyo anaechunga utekelezaji wako wa haki ya kazi yako au kutotekeleza kwako na uzembe wako.
Ikiwa miongoni mwa mambo muhimu ambayo mwenye kufunga anatakiwa achunge sana ni kula chakula cha halali na kujibiwa dua, anapaswa atambue kuwa anapochukua ujira na akawa hajatekeleza wajibu wake ipasavyo hakika yeye anakula kisicho chake na anakula Haramu kwani yeye atakuwa ni mtu aliyechukua malipo bila ya kufanya kazi yake, au atakuwa amevunja mkataba wa kazi na ahadi yake ya kazi pamoja na Masharti ya kazi, iwe kazi hiyo ni ya Serikali au ya Mtu binafsi.

Na ninaisema kauli yangu hii, na ninamwomba msamaha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ajili yenu na kwa ajili yangu.

*   *   *

**Sifa zote njema ni zake mwenyezi Mungu Mtukufu Mlezi wa viumbe vyote. Na rehma na amani ziwe juu ya Mtume wa Mwisho katika Mitume, na Manabii wake Mwenyezi Mungu Mtukufu, Bwana wetu Muhammad S.A.W, na Jamaa zake, na Maswahaba wake wote, na atakayewafuata kwa Wema mpaka siku ya Malipo.**

Ndugu zangu Waislamu.

Hakika ya Kazi na Ibada ni kitu kimoja kama matawi mawili ya mti mmoja, kwani Ibada ni kazi, na Kazi safi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa hiyo kazi na Ibada hazitengani.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

**{وَقُلِ اعْمَلُواْ فَسَيَرَى اللّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُ وَالْمُؤْمِنُونَ وَسَتُرَدُّونَ إِلَى عَالِمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ}**

{Na sema: Tendeni vitendo. Na Mwenyezi Mungu, na Mtume wake, na Waumini wataviona vitendo vyenu. Na mtarudishwa kwa Mwenye kujua siri na dhaahiri; naye atakuambieni mliyo kuwa mkiyatenda}.

Na Mzingativu wa Sira ya Mtume S.A.W na Sira ya Maswahaba wake R.A, baada yake, na katika Historia yote ya Uislamu, ataona kwamba Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ni Mwezi wa Kazi na Uzalishaji, bali

shinde nyingi za Kiislamu zilikuja ndani ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani uliobarikiwa. Mwezi huu kwa hakika ni wa shinde nyingi za Waislamu pamoja na Funguzi. Kwani ndani ya Mwezi huu wa ramadhani, ulipatikana Ushindi wa vita vikuu vya Badri, ambavyo vilikuwa ni mapambano tenganishi ya Haki na Batili, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliwakirimu Waumini kwa Ushindi kutoka kwake, kwa uchache wa idadi yao na vifaa vyao.

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu:
{وَلَقَدْ نَصَرَكُمُ اللَّهُ بِبَدْرٍ وَأَنْتُمْ أَذِلَّةٌ  فَاتَّقُوا اللَّهَ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ * إِذْ تَقُولُ لِلْمُؤْمِنِينَ أَلَنْ يَكْفِيَكُمْ أَنْ يُمِدَّكُمْ رَبُّكُمْ بِثَلَاثَةِ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُنْزَلِينَ * بَلَى إِنْ تَصْبِرُوا وَتَتَّقُوا وَيَأْتُوكُمْ مِنْ فَوْرِهِمْ هَذَا يُمْدِدْكُمْ رَبُّكُمْ بِخَمْسَةِ آلَافٍ مِنَ الْمَلَائِكَةِ مُسَوِّمِينَ * وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَى لَكُمْ وَلِتَطْمَئِنَّ قُلُوبُكُمْ بِهِ  وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِنْدِ اللَّهِ الْعَزِيزِ }.

{Na Mwenyezi Mungu alikwisha kunusuruni katika Badri nanyi mlikuwa wanyonge. Basi mcheni Mwenyezi Mungu ili mpate kushukuru. Ulipo waambia Waumini: Je, haitakutosheni ikiwa Mola wenu atakusaidieni kwa Malaika elfu tatu walio teremshwa? Kwani! Ikiwa mtavumilia na mkamchamngu na hata maadui wakikutokeeni kwa ghafla, basi hapo Mola wenu Mlezi atakusaidieni kwa Malaika elfu tano wanao shambulia kwa nguvu. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila kuwa ni bishara kwenu, na ili nyoyo zenu zipate kutua. Na msaada hautoki isipo kuwa kwa Mwenyezi Mungu, Aliye tukuka, Mwenye nguvu na Mwenye hikima}.}

Na katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Ufunguzi wa Makkah ulifanyika na ulikuwa Mkubwa, na Mwenyezi Mungu Mtukufu alimpa cheo kikubwa Mtume wetu Muhammad S.A.W kwa Ufunguzi huo,

pamoja na Waumini, na akawafedhehesha Makafiri na Washirikina. Na katika zama hizi, ulipatikana Ushindi wa tarehe kumi Mwezi wa Ramadhani, sawa na sita Oktoba ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliiwafikisha Misri, ambapo ilirejesha Ardhi yake na Heshima yake, na kauli mbiu ya wanajeshi ilikuwa: Mwenyezi Mungu Mtukufu ni Mkubwa, pamoja na kufunga, kufanya Ibada za Usiku na Kusoma Qurani na Kusoma Dua 6a Kweli, ukapatikana Ushindi wa wazi, na Maadui wakatimuliwa kwa ajili ya kuilinda Dini,Nchi, Ardhi na Heshima, na hili lilikuwa somo la kiutendaji kwa kile mwenye kuwa na wazo katika nafsi yake la kutaka kuishambulia Misri. Hakuna kinachotuzuia kurejesha moyo wa Ramadhani katika nyanja zote za maisha yetu ili tufanikiwe na kuimarisha Nguzo za Haki na Uadilifu, na kulinda Ardhi na Heshima pamoja na Utukufu wake, mpaka turejeshe nafasi ya Umma wetu na uzito wake baina ya Mataifa, na haiwi hivyo isipokuwa kwa kuunganisha nguvu zetu na kuwa kitu kimoja na kuwa na kauli moja, na kulizunguka lengo moja, kwa juhudi, bidii na Kazi zaidi, na kuwaletea heri watu wote

Ewe Mola wetu tubariki sisi katika Mwezi Mtukufu wa Shaabani, na utufikishe katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na utukubalie amali zetu ndani ya Mwezi huo, Ewe Mlezi wa Viumbe vyote.Na Dua yetu ya mwisho ni Alhamdulillahi Rabi Alaalameen.